Jina:____________________ Namba Yako ________________

**7015/2**
**KISWAHILI**
**Desemba 2009**
**Saa 1½**

Sahihi ya Mtahiniwa ________________

Tarehe ________________

**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# CERTIFICATE IN EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT AND EDUCATION

KISWAHILI

**Saa 1½**

http://college.manyamfranchise.com

**MAAGIZO**

*Karatasi hii ina sehemu tatu: Insha, Ufahamu na Lugha.*
*Chagua insha moja kati ya mbili ulizopewa.*
*Jibu maswali yote ya ufahamu na lugha.*
*Jibu maswali matatu.*

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 20 | |
| Jumla | 50 | |

**Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

*© 2009 The Kenya National Examinations Council*

## SEHEMU YA KWANZA: INSHA (Alama 15)

*Jibu swali 1 au 2*

Andika insha moja isiyopungua maneno 300 kuhusu mojawapop ya mada zifuatazo:

1. Mwandikie barua mfadhili wako ukimshukuru kwa kuyadhamini masomo yako katika chuo cha ualimu.

2. Andika insha inayomalizika kwa:

   "Nilipoyatazama maisha yangu ya kisogoni, sikuwa na budi kumshukuru Mungu kwa kuninusuru."

http://college.manyamfranchise.com

## SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (ALAMA 15)

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Lugha ni mojawapo ya rasilimali muhimu katika maisha ya binadamu. Pamoja na kuwa lugha ni kitambulishi cha utamaduni wa jamii mahususi, lugha imetumiwa na binadamu kwa miongo mingi kama nyenzo ya kuwasilisha hisia za moyoni kupitia kwa tungo kama vile mashairi. Hali kadhalika, lugha hutumiwa na binadamu kuwasilisha haja yake kwa binadamu mwenzake. Si ajabu basi kwamba, hata mtoto anapozaliwa huashiria kutoridhika kwake na ulimwengu mpya kwa kulia; hii ndiyo lugha anayofahamu ati.

Aidha, lugha ni kipengele muhimu cha kudumisha umoja na mshikamano wa kitaifa. Watu ambao huzungumza lugha moja ya taifa kama vile Kiswahili hujenga udugu miongoni mwao. Watu hawa, hata wanapokutana ugenini, wao hujihesabu kuwa watu wa aila moja licha ya tofauti za kiusuli ambazo huenda zikajitokeza.

Lugha ni chombo muhimu cha kufafanulia na kuenezea sera za kiutawala. Mathalan, lugha ya Kiswahili nchini humu imetumiwa kuwaelimisha wananchi katika sehemu mbalimbali kuhusu mbinu za kujikwamua kiuchumi. Vilevile Kiswahili kimetumiwa kuendeshea kampeni za kupambana na magonjwa sugu. Kupitia kwa kampeni hizi, wananchi wamehamasishwa kuhusu umuhimu wa kuzingatia lishe bora, kudumisha usafi wa mazingira ili kujikinga dhidi ya magonjwa yanayasababishwa na uchafu na kadhalika.

Lugha ni chombo cha kupitisha maarifia na nasaha. Mwalimu kwa mfano hutumia lugha kumfafanulia mwanafunzi mada mbalimbali. Pia, kupitia kwa methali na semi nyingine, wanajamii hupitisha maarifa mbalimbali na hekima kwa vijana. Si ajabu kumsikia mzee akimhimiza kijana kukabiliana na changamoto za maisha bila kukata tamaa kwa kumwambia, "papo kwa papo kamba hukata jiwe." Almuradi kila jamii ina mbinu zake za kutumia lugha ili kupitisha thamani zake kwa vizazi mbalimbali. Pamoja na kuwa lugha ndiyo nyenzo kuu ya kujenga na kudumisha mahusiano ya kijamii, ni muhimu kukumbuka kwamba lugha huweza kutumiwa kama chombo cha kutenganisha. Hili

http://college.manyamfranchise.com

huweza kutokea iwapo lugha itatumiwa kiholela.

Kila mzungumzaji wa lugha fulani hana budi kuelewa kuwa zipo kaida ambazo huongoza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano, mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi, mzee na kijana n.k. yanamhitaji kila mshiriki katika mazungumzo hayo kutumia lugha ya adabu. Kadhalika, lugha huweza kuwa chombo cha kuleta mafarakano ikiwa itatumiwa na watu kama njia ya kueneza kashfa kuhusu wanajamii wenzao, ambao huenda wakawa na mitazamo tofauti na ile yao.

Maswali

(a) Huku ukirejelea taarifa, thibitisha kuwa lugha ni chombo cha kuwasilisha hisia. (alama 2)

http://college.manyamfranchise.com

(b) Fafanua umuhimu wa lugha katika kudumisha maendeleo ya kijamii kwa mujibu wa kifungu. (alama 5)

(c) Eleza msimamo wa mwandishi kuhusu suala la matumizi ya lugha. (alama 5)

(d) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa.

(i) sera ______________________________

______________________________

(ii) nasaha ______________________________

______________________________

(iii) Kaida ______________________________

______________________________

(alama 3)

## SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 20)

***Jibu maswali <u>yote</u> katika sehemu hii.***

http://college.manyamfranchise.com

(a) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

"Nitampendekezea mbunge wetu jambo hili." Mandu akasema. (alama 2)

______________________________

______________________________

(b) Tambulisha matumizi ya kiambishi <u>ku</u> katika sentensi:
Meto ameahidi kuwa ata<u>ku</u>saidia. (alama 1)

______________________________

______________________________

(c) Tunga sentensi kubainisha aina zifuatazo za maneno:

(i) Nomino dhahania

______________________________

(ii) Kivumishi kionyeshi

______________________________

______________________________

(alama 4)

(d) Andika sentensi ifuatayo katika jinsi ya kutendwa.
Waumini wengi walikuwa wakitembelea madhabahu hayo. (alama 2)

(e) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.
Ngozi za ng'ombe hao ziliuzwa jana. (alama 2)

(f) Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi:
Mumbi atawaalika wengine. (alama 2)

(g) Andika sentensi upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa vinyume.
Topasi aliniomba nikusanye taka hizo. (alama 2)

(h) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana mbili za neno 'kucha'. (alama 2)

(i) Andika methali yenye maana sawa na: Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. (alama 2)

j) Ndama ni kwa ng'ombe, ________________ ni kwa ndege. (alama 1)

http://college.manyamfranchise.com